**PRIMARY EDUCATION SERVICES NETWORKING ORGANIZATION (PESNO)**

**SIMU: 0713- 526533**

**0767- 526533**

# MTIHANI WA PILI WA UTAMILIFU KWA DARASA LA SABA

# SOMO: HISABATI [02]

**TAREHE 04/05/2021 MUDA: MASAA 2**

**JINA LA MTAHINIWA:** ____________________________________________

**JINA LA SHULE:** ____________________________________________________

**WILAYA**: ____________________ **MKOA:** _____________________

## MAELEKEZO:

1. Jaza nafasi wazi hapo juu na katika karatasi ya kujibia
2. Jibu maswali yote kwa kufuata maelekezo katika kila sehemu.
3. chagua jibu sahihi kisha siliba herufi yake katika karatasi ya kujibia (OMR)kwa kutumia kalamu ya risasi kuanzia swali 1 hadi 40
4. Katika swali la 41 hadi 45 jibu maswali kwa kuandika majibu nyuma ya (OMR) kwa kutumia kalamu ya wino, hakikisha unaonyesha njia.
5. Hakikisha kazi yako iko nadhifu na safi
6. Mtihani huu una kurasa nne zilizochapishwa

SEHEMU A : MASWALI YA KUCHAGUA.

Kwa swali la 1 – 40 kokotoa na changua jibu sahihi kisha siliba herufi yake kwenye karatasi maalumu ya kujibia uliyopewa **(OMR)** ukitumia penseli ya **HB tu**.

1. Tafuta jumla ya thamani ya trakimu 7 na 9 katika namba 9087006.
   A. 900700 D. 970000
   B. 9000700 E. 90700
   C. 9007000

2. Fupisha "800000 + 0 + 9000 + 0 + 0 + 9".
   A. 899 D. 809009
   B. 800909 E. 908009
   C. 80909

3. Tafuta thamani ya tarakimu 6 katika namba 34.261
   A. 0.06 D. 600
   B. 60 E. 0.006
   C. 0.6

4. Badili $\frac{74}{7}$ kuwa sehemu mchanganyiko.
   A. $1\frac{4}{7}$ D. $10\frac{7}{4}$
   B. $7\frac{4}{7}$ E. $10\frac{4}{7}$
   C. $7\frac{4}{10}$

5. Panga number zifuatazo kwa mfumo wa ndogo kwenda kubwa; **$\frac{2}{3}$, 0.6, $\frac{3}{4}$, $\frac{4}{5}$, 1, 0.5**
   A. $\frac{4}{5}$, ¾, $\frac{2}{3}$, 0.6, 0.5
   B. 0.5, 0.6, $\frac{2}{3}$ , ¾, $\frac{4}{5}$,1
   C. $\frac{2}{3}$, 0.5, 0.6, ¾, $\frac{4}{5}$
   D. 0.5, 0.6, $\frac{2}{3}$, ¾, $\frac{5}{5}$
   E. 0.5, 0.6, $\frac{2}{3}$, $\frac{4}{6}$, ¾

6. Badili MMIV kuwa numeral za kawaida.
   A. 204 D. 2009
   B. 1004 E. 2005
   C. 2004

7. Badili 8.08% kuwa desimali; jibu liwe katika nafasi tatu za desimali.
   A. 0.081 D. 0.0808
   B. 0.008 E. 0. 088
   C. 0.808

8. 56 – 72 + 44 =
   A. – 28 D. 18
   B. 44 E. 28
   C. 18

9. 8.36 + 11.7 =
   A. 19.43 D. 9.53
   B. 20.06 E. 20.53
   C. 20.43


10. 567 x 1000 =
    A. 56700 D. 567000
    B. 765000 E. 657000
    C. 5670

11. $15\frac{3}{4} \div 10\frac{1}{2} =$
    A. $1\frac{1}{2}$ D. $\frac{2}{3}$
    B. $2\frac{1}{2}$ E. $1\frac{1}{3}$
    C. $\frac{1}{2}$

12. $^-96 - {}^-490 - {}^+4 =$
    A. $^-390$ D. $^+296$
    B. $^-296$ E. $^+390$
    C. $^-590$

13. $46 - 42\frac{5}{7} =$
    A.$4\frac{5}{7}$ D. $3\frac{5}{7}$
    B. $3\frac{2}{7}$ E. $4\frac{2}{7}$
    C. $90\frac{5}{7}$

14. Andika namba inayoweza kupatikana kutokana na **mchoro** hapo chini..




    A. 3245 D. 32405
    B. 302 405 E. 320450
    C. 320,405

15. $^-3 \times {}^-2 \div {}^-1 =$
    A. $^+6$ D. $^-6$
    B. $^-3$ E. -1
    C.$^+3$

16. Tafuta namba inayokosekana katika mfululizo huu;
    $^-64$, $^+16$, $^-4$, _____
    A· $^-1$ D. ¼
    B. $^-16$ E. $^+4$
    C. $^+1$

17. Je, nini tofauti kati ya $18^2$ na $17^2$?
    A. 18 D. $35^2$
    B. 17 E. 35
    C. $1^2$

18. Tafuta kipeuo cha pili cha nusu ya zao la 50 na 400.

A. 1000 D. 100
B. 200 E. 40
C. 400

19. Ni kundi lipi linawakilisha vigawo tasa vya 45?

A. 1, 3 and 5 D. 3 and 15
B. 3 and 5 E. 2, 3 and 5
C. 1, 3, 5 and 15

20. Tafuta jumla ya Kigawo Kikubwa cha shirika (KKS) na kigawe kidogo cha shirika (KDS) vya 39, 78 na 156.

A. 195 D. 157
B. 159 E. 39
C. 156

21. Badili saa 6:01 mchana kuwa katika mfumo wa masaa 24.

A. Saa 1201 D. Saa 1012
B. Saa 0001 E. Saa 0012
C. Saa 2401

22. Badili $78\frac{3}{5}$ kuwa katika asilimia.

A. 786% D. 78.60%
B. 78.6% E. 7806%
C. 7860%

23. Je, kuna wiki ngapi katika miaka 4 ½ ?

A. Saa 216 D. Saa 208
B. Saa 52 E. Saa 234
C. Saa 48

24. Gawanya Sh. 12000 na senti 90 kwa 30

A. sh. 3 400cts D. sh. 400 03cts
B.sh. 400 senti 30 E. Sh. 400 senti 90
C. Sh 400 senti 40.

25. Ikiwa; p = 3.45, q = 0.69. Je, thamani ya p itakuwa ngapi ikiwa q = 1.38?

A. 0.69 D. 6.9
B. 9.6 E. 0.069
C. 0.96

26. Seremala alitengeneza meza kwa gharama ya Sh. 250000; ikiwa alipata faida ya 10% . alipata kiasi gani kwa kuuza meza hiyo?

A. Sh. 25000 D. Sh. 225000
B. Sh. 250000 E. Sh. 200000
C. Sh. 275000

27. Gawa miaka 18 na wiki 39 kwa 5.

A. miaka 3 wiki 39 D. miaka 3 wiki 37.5
B. miaka 39 wiki 3 E. miaka 2 wiki39
C.miaka 2 wiki 37.5

28. Akitumia gari yake ya 504; Samata alisafiri umbali wa km 30 ndani ya masaa2 ½. Tafuta mwendokasi wake (jibu katika $\frac{Km}{saa}$)


A. $90\frac{km}{saa}$ D. $12\frac{km}{saa}$
B. $60\frac{km}{saa}$ E. $15\frac{km}{saa}$
C. $18\frac{km}{saa}$

29. Chriss-Nelly hutumia masaa 2 na dakika 15 kujisomea kila siku. Ikiwa alianza saa 1:15 jioni; alimaliza kujisomea saa ngapi? (Jibu katika mfumo wa masaa 24)

A. saa 0915 D. saa 2115
B. saa 2130 E. saa 0915
C. saa 1915


30. Tafuta mzingo wa umbo lifuatalo.

A. sm 40
B. sm 33
C. sm 59
D. sm 61
E. sm 47





31. Tafuta thamani ya pembe **PQS.**

A. $40^0$
B. $120^0$
C. $30^0$
D. $80^0$
E. $100^0$





32. Kwa kutumia mchoro ufuatao andika majira ya nukta U.

A. (- 2, 0)
B. (0, - 3)
C. (+3, -3)
D. (– 3,0)
E. (- 3, - 3)





33. Tafuta eneo la umbo ifuatao.

A. $sm^2 140$
B. $m^2 70$
C. $sm^2 70$
D. $sm^2 84$
E. $sm^2 96$




34. Tafuta ujazo wa mche mstatili ufuatao.

A. $sm^3$ 1800
B. $sm^3$ 800
C. $sm^3$ 1500
D. $sm^3$ 1200
E. $sm^3$ 18000



35. Mzee Ntagondwa aliwagawia wanae watatu ng'ombe kama ifuatavvo; Kadudu alipata $\frac{1}{3}$ ya ng'ombe wote, Daniel nusu ½ waliobakia. Ikiwa Toto alipata ng'ombe 80, Kadudu na Daniel walipata ng'ombe wangapi kutoka kwa baba yao?
A. ng'ombe 80 D. ng'ombe 400
B. ng'ombe 240 E. ng'ombe 160
C. ng'ombe 120

36. Amina hununua lita 5 za maziwa kwa ajili ya mgahawa wake kila siku. Ikiwa kila lita huuzwa Sh. 1500; atatumia kiasi gani katika mwezi wa Aprili?
A. Sh. 250000 D. Sh. 205000
B. Sh. 22500 E. Sh. 225000
C. Sh. 2250000

37. Duwasa waligawa lita 1480000 kwa kaya 2500. Ikiwa kila kaya ilipokea kiasi sawa, kila kaya ilipata lita ngapi za maji?
A. lita 592 D. lita 5920
B. lita 562 E. lita 5820
C. lita 582

38. Devereva wa Bajaj aliingia mkataba wa kuwasilisha Tsh. 70000 kwa wiki. Baada ya wiki ngapi atamaliza deni la Tsh. 7000000?
A. wiki 10 D. wiki 70
B. wiki 100 E. wiki 700
C. wiki 1000

39. Magoli alivuna tani 60 za mahindi 1990. Aliuza tani 58 @ Sh. 1000000. Baadaye alinunua trekta kwa Sh. 35000000; je, alibakiwa na kiasi gani cha pesa?
A. Sh. 25000000 D. Sh. 23000000
B. Sh. 35000000 E. Sh. 22000000
C. Sh. 58000000


40. Mama Daudi ana watoto watatu; kila mtoto hutumia robo kilo ya mchele kwa siku. Je, watatumia gramu ngapi za mchele kwa wiki nne?
A. gramu 21 D. gramu 750
B. gramu 7000 E. gramu 2100
C. gramu 21000

## SEHEMU B : MASWALI YA KUKOKOTOA


Kwa swali namba 41 – 45. Kokotoa kwa makini ukionyesha njia vizuri kwenye karatasi ya kujibia ukitumia kalamu ya **bluu au nyeusi** tu.

41. Tafuta thamani ya x katika: $7x + 3 - 6x = 0.5x + 6$

42. Mchoro ufuatao unaonyesha mgawanyo wa alama alizopata Daniel kwenye mtihani wa Utamilifu mwaka 2020. Ikiwa alipata $\frac{40}{50}$ katika Hisabati; alipata alama ngapi katika somo la Kiingereza?




43. ikiwa mzingo wa umbo ABCD ni sm 40; Tafuta eneo lake.




44. Umri wa Doreen ulikuwa 0.2 ya umri wa baba yake miaka 4 iliyopita. Je, Doreen atakuwa na umri gani miaka miwili ijayo ikiwa umri wa baba wa sasa ni mara 4 ya umri wake?

45. Zomboko alinunua makasha 10 ya nyanya Jumatatu, makasha 15 Jumanne, makasha 20 Jumatano na makasha 12 Alhamis. Ikiwa wastani wa makasha 15 yalinunuliwa kwa siku tano mfululizo. Alinunua makasha mangapi siku ya Ijumaa?